

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UTEUZI WA WAGOMBEA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA KATA 13

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13 (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura Na. 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata 13 za Tanzania Bara uliopangwa kufanyika tarehe 17 Agosti mwaka 2019.

Tume ilitangaza kutoa Fomu za Uteuzi wa Wagombea kuanzia tarehe 29 Julai hadi 03 Agosti, 2019 na Siku ya Uteuzi ilipangwa kuwa tarehe 03 Agosti, 2019.

Hadi kufikia tarehe 03 Agosti, 2019 saa 10:00 jioni muda wa mwisho wa kurejesha Fomu za Uteuzi, ni wagombea 13 kutoka Chama cha Mapinduzi ndiyo waliokuwa wamerejesha Fomu za Uteuzi.

Kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 45 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura Na. 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewateua wagombea hao 13 kuwa wagombea katika Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata 13 za Tanzania Bara.

Imetolewa tarehe 03 Agosti, 2019 na:

Hussein Makame

AFISA HABARI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI